# NENO LA X- MAS – 25 DEC. 2022
# MAANA KWA AJILI YETU MTOTO (YESU) AMEZALIWA
## MAANDIKO: MWANZ. 3:15, ISAY. 7:14, 9:6 NA MATH. 1:18-22.

1. **UTANGULIZI**

   Nabii Isaya anatabiri wazi kwamba sehemu kubwa ya huduma ya masihi atakayezaliwa (Yesu) atahudumu Galilaya ambayo ilikuwa ni Mkoa katika nchi ya Israeli ambao watu wake walidharauliwa sana na hasa kutokana na kazi yao ya kuvua samaki tu maisha yao yote na ambao hawakujishughulisha na Elimu wala mambo yoyote ya utawala katika Taifa la Israeli ( ni mfano wa kabila la **Waazabe** au **Wabarabaigi** katika nchi ya Tanzania) " Tuangalie ***Math. 4:12-25.***

   **Note:** Galilaya ilijulikana (ilisifika) kwa kudharauliwa na Wayahudi na watu wake walikuwa ni watu wa dhiki (walikuwa na maisha magumu na wala hapakuwa na maendeleo yoyote, wao walifahamu kuvua samaki kama kitoweo na siyo kuuza ili wapate fedha, hawakuwa na nyumba nzuri, hakukuwa na barabara nzuri na watawala katika Israeli hawakujishughulisha kabisa na Galilaya; magonjwa na vifo vingi vilikuwa katika Galilaya maana hakuna Hospitali za watu kujifungulia!! Au kutibiwa malaria maana Galilaya kwa sababu ya kuzungukwa na Ziwa Galilaya, kulikuwa na mbu wengi sana wakati huo!!

2. Mwanafunzi wa kwanza wa Yesu Kristo alikuwa ni Yohana Mbatizaji (mtoto wa Kuhani Zakaria). ***Yoh. 1:32-34*** ambaye alikuwa anaishi nchi ya Galilaya katika nyika ya milima ya Golamu ambako ndiko chanzo cha mto Yordani kinakotokea, Baadaye ndipo wanafunzi wake Yohana wawili (yaani Andrea na nduguye Petro waliomsikia Yohana akinena habari za Yesu,

walimwacha Yohana na kumfuata Yesu. (Ukisoma historia ya Yohana Mbatizaji na vaa yake, na chakula chake alichokuwa anakula na maisha yake kwa ujumla ya kutojulikana anaishi na kulala wapi, ni wazi kabisa kwamba wanafunzi wake wa kwanza (kina Andrea, Simoni, Filipo) waliokuwa wote wanatoka Galilaya na walikuwa wanafanana fanana kimaisha na Baba yao wa Imani Yohana Mbatizaji ***( Yoh. 1:35-43). Math. 3:4***

- Filipo alipojaribu kumshuhudia Nathanaeli msomi huyu, yeye alishangaa na kumuuliza Filipo " Laweza NENO jema kutoka Nazareti? ***(Yoh. 1:44-46)*** swali lake hili lilitokana na historia aliyo nayo kwamba Masihi (mtawala) katika Isareli lazima atokee katika kabila la Yuda ambalo maskani yake ni Yerusalemu katika mji mdogo wa Bethlehemu (km. 16) kutoka mjini Yerusalemu wa sasa. **Yoh. 7:40-43.**

- Wanatheolojia wengi wanakubaliana kwamba Filipo alifahamiana sana na Nathanaeli ambaye hakuwa mwenyeji wa Galilaya alipokuwa na yeye amepata neema ya kwenda kusoma katika shule za Kiyahudi zilizo nje ya Galilaya na wakawa marafiki waliopendana na ambao walishika torati kwa dhati kabisa kama walivyofundishwa na Mafarisayo wao.

3. Baada ya kukupatia japo kwa muhutasari picha ya watu wa Galilaya jinsi maisha yao yalivyokuwa na jinsi walivyodharauliwa. Yesu anachagua kwenda kuishi katika maeneo haya ya Galilaya na kisha kubadilisha kabisa historia ya Galilaya!! **Kuna mambo kadhaa Yesu aliyoyafanya wakati alipokuwa anaishi Galilaya yaliyosababisha historia yao ibadilike kabisa.**

a. Yesu aliinua watumishi wakuu sana waliotumiwa na Bwana kwa ishara kubwa kutoka Galilaya ambao walizima kabisa tambo za Wayahudi waliokuwa wanajivua kwamba wamesoma (Mafarisayo

na Masadukayo) na kudharau wengine na kushika torati. ***Mdo. 4:13-14.*** " Petro alikuwa anaitwa Simoni (yaani Unyasi) Ki-Ebrania, Yesu akambadilisha kabisa na kumwita Petro (PETRA) kipande cha mwamba, na akampa mamlaka ya kuwa msimamizi wa huduma yake (Askofu Mkuu). ***Yoh. 21:15-17, Luk. 22:31-32 na Mdo. 5:12-16.*** (Wayahudi walitamani hata kivuli cha Petro kiwaangukie wagonjwa wao na wakapona!!)

b. Yesu aliponya wagonjwa wengi sana Galilaya kuliko sehemu nyingine nyingi katika Israel na hivyo kupelekea watu hawa waliokuwa katika dhiki kwa muda mrefu kwa kukosa huduma ya uponyaji **kuchangamka** na kufurahia maisha na wao. ***Isay. 9:1-3, Filip. 4:4*** " Hakuna jambo muhimu sana kwa binadamu kama **kufurahi (unawezakuwa na fedha au cheo au ndoa au watoto au nyumba au gari n.k lakini kama huna furaha, huna changamko la moyo, yote hayo ni kazi bure. *Zab.119: 111.***

   **Note: Graph ya vifo katika Galilaya ikashuka mno!! "** Huu ndiyo mzigo mmojawapo uliojaa sana ndani ya moyo wangu (kushusha kabisa graph ya wapendwa wasife hovyo hovyo kabla ya wakati wa Mungu; pamoja na kuleta **CHANGAMKO** halisi linalotoka ndani ya moyo kwa watoto wa Mungu.

c. **Tuseme sote " Maana kwa ajili yetu mtoto Yesu amezaliwa, ambaye uwezo wa Kifalme uko mabegani mwake".** Alipokaa Galilaya, uwezo wake wa Kifalme ulibadilisha kabisa hali ya uchumi kwa wenyeji wa Galilaya- walizoea kuvua samaki wachache mno kama kitoweo, wakaanza kuvua samaki wengi hadi kuwauza na kupata faida. ***Luk. 5:1-11, Yoh. 21:1-14***. Yesu alionyesha kujali sana na kujishughulisha na mahitaji yao ya mwilini pia ikiwa ni pamoja na kuwaonyesha kwamba hata kifungua kinywa (Break Fast) ni mlo muhimu sana. Hivi

tunadhani kwamba Yesu aliwapa mkate wale pamoja na samaki wa kuokwa wale bila kitu kingine cha kulainishia!! Hakika wangekwamwa!!

- Hata uchumi wa wanafunzi wake alihakikisha unapanda mara mia moja kuliko walivyokuwa kwanza kabla ya kumtumikia. ***Math. 19:27-30.*** Tunaposherekea X- MAS 2022 tuamini Yesu (mtoto) amezaliwa kwa ajili yetu, anayo mamlaka ya kubadilisha uchumi wetu na historia zetu, amezaliwa kwa ajili yetu!!

- Wale **waliotudharau**, hawatatudharau tena, amekuja Yesu kututoa katika dhiki zetu na kutwaa udhaifu wetu pamoja na magonjwa yetu!! ***Math. 8:7.***
  “Tuseme sote**, mtoto Yesu amezaliwa kwa ajili yetu, ambaye uweza wa Kifalme (uweza wa kubariki, kuponya, kuinua) uko mabegani mwake, yeye ni mshauri wa ajabu (Extra Ordinary Wisdom (Wonderful Counselor).** ***Yoh. 2:5-11, Luk. 5:4-8,*** **tena mtoto Yesu ndiye Mfalme wa amani yetu; hata kama sina nguo mpya ya sikukuu au chakula kipya, maadamu ndani yangu nina Yesu yeye ni amani yangu tosha kabisa; yeye ni zaidi ya utajiri wote na nguvu ya kusonga mbele na wokovu pasipo kuzimia njiani.** ***Isaya. 9:1-3.*** **Amina.**

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***X –MAS***
***25/12/2022***